

## Ridhaa kutoka kwa Mzazi ya kushiriki kwenye Utafiti

Unaombwa kumruhusu mtoto wako kushiriki kwenye uchunguzi wa kitafiti. Kabla haujakubali, ni lazima upewe muhtasari wa utafiti. Muhtasari huu utakuwa na taarifa muhimu zitakazokusaidia kuelewa sababu zitakazokufanya aidha ukubali mtoto wako ajiunge au uchague asijiunge na utafiti.

Kabla ya kukubali, mpelelezi lazima akueleze kuhusu:

- (i) Sababu, mbinu na muda wa utafiti.
- (ii) Mbinu zozote ambazo ni za kimajaribio
- (iii) Hatari za msingi zionekanazo, masumbufu na faida za utafiti
- (iv) Uwezekano wowote wa matibabu au taratibu mbadala zenye faida
- (v) Jinsi usiri utakavyodumshwa; na
- (vi) Nani wa kuwasiliana naye kwa maswali, malalamiko na majeraha

Ambapo itatakiwa, mpelelezi atalazimika kukwambia pia kuhusu:

- (i) Fidia zozote zilizopo au matibabu iwapo jeraha litatokea.
- (ii) Uwezekano wa hatari zisizoonekana.
- (iii) Mazingira ambayo mpelelezi atasimamisha ushiriki wa mtoto wako.
- (iv) Gharama zozote zitakazongezeka kwako au kwa mtoto wako.
- (v) Kitakachotokea ukiamua kusitisha ushiriki wa mtoto wako.
- (vi) Lini utakapo ambiwa kuhusu uvumbuzi mpya ambao utaathiri utayari wako kumruhusu mtoto wako kushiriki.
- (vii) Idadi ya watu watakaokuwepo kwenye uchunguzi; na
- (viii) Jinsi utakavyohitajika kuidhinisha matumizi ya taarifa za matibabu za mtoto wako kwa ajali ya utafiti

Ushiriki wa mtoto wako kwenye utafiti huu ni wa hiari, na hautaadhibiwa wala kupoteza faida kama ukikataa mtoto wako kushiriki au ukiamua kusitisha ushiriki. Kutia sahihi waraka huu inamanisha kuwa utafiti, ukijumlisha taarifa za hapo juu, zimeelezwa kwako kwa mdomo na kwamba umekubali kwa hiari mtoto wako ashiriki. Kama umekubali kushiriki, ni lazima ukabidhiwe nakala ya waraka huu iliyotiwa sahihi na muhtasari wa utafiti ulioandikwa kwa kiingereza.

### Maswali?

Kama una maswali yoyote, malalamiko, majeraha au jambo lolote kuhusu utafiti, unaweza wasiliana na mpelelezi kwa kutumia namba za simu zilizoainishwa kwenye muhtasari wa utafiti ulioandikwa. Kama unaswali kuhusu haki za mtoto wako kama mshiriki au una maswali, malalamiko, majeraha au jambo ambalo unahisi huwezi jadili na mpelelezi, tafadhali wasiliana na ofisi ya Bodi ya taasisi ya Ukaguzi kwa kutumia namba ya simu au anwani ya barua pepe iliyopo kwenye muhtasari wa utafiti.

\_\_\_\_\_  
Jina la Mtoto

\_\_\_\_\_  
Jina la Mzazi/Mlezi

\_\_\_\_\_  
Sahihi ya Mzazi/Mlezi

\_\_\_\_\_  
Tarehe

\_\_\_\_\_  
Uhusiano wa Mzazi/Mlezi wa Mtoto

Ninaidhinisha ya kwamba nilikuwepo kama mkalimani kwa kipindi chote cha mchakato wa ridhaa kwa ajili ya utafiti huu. Ninaidhinisha ya kwamba ninastahili na ujuzi wote unaohitajika kutoa tafsiri kati ya Kiingereza na lugha ya mwamali. Kwa kutia sahihi katika fomu hii, ninaidhinisha ya kwamba nimetoa tafsiri yote na iliyokamili ya mazungumzo kati ya mtafiti kupokea ridhaa na mwamali, kwa kadiri ya uwezo wangu.

\_\_\_\_\_  
Jina la Mkalimani

\_\_\_\_\_  
Sahihi ya Mkalimani

\_\_\_\_\_  
Tarehe